

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
KURUGENZI YA MAWASIIIANO YA RAIS IKULU

Simu: 255-262961500/1
Nukushi: 255-262961502
Barua pepe : press@ikulu.go.tz
Tovuti : www.ikulu.go.tz



OFISI YA RAIS,
IKULU,
1 BARABARA YA JULIUS NYERERE,
CHAMWINO,
S.L.P 1102,
40400 DODOMA.

Dar es Salaam
22 Oktoba, 2022

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan, amefanya uteuzi wa Wenyeviti wa Bodi kama ifuatavyo:-

A: WENYEVITI WA BODI:

- 1) Amemteua Dkt. Florens Martin Turuka, Katibu Mkuu Mstaafu kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART). Aidha, amewateua Maofisa watano (05) kuwa Wajumbe wa Bodi ya DART kama ifuatavyo:-
 - (i) Zainab Salome Msimbe, Mhasibu Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali;
 - (ii) Mhandisi Johansen Jonathan Kahatano, Mkurugenzi wa Barabara, Mamlaka ya Udhubiti wa Usafiri wa Ardhini (LATRA);
 - (iii) Bw. Aron Johnson Kisaka, Mkurugenzi wa Huduma za Usafirishaji, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi - Dodoma;
 - (iv) Bw. Benjamini Kiloba Dotto, Mkurugenzi wa Miundombinu, Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA); na
 - (v) Bi. Mwantumu Mshirazi Salim, Katibu wa Kampuni, *Export Processing Zone Authority (EPZA)*, Dar es Salaam.
- 2) Amemteua Bi. Beng'i Mazana Issa kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa. Bi. Beng'i ni Katibu Mtendaji, Baraza la Taifa la Uwezesaji Wananchi Kiuchumi (NEEC).

Vile vile, amewateua Maofisa watano (05) kuwa Wajumbe wa Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa kama ifuatavyo:-

- (i) Dkt. Hemed Aziz Mpili, Afisa Ugavi Mwandamizi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI);
- (ii) Prof. Provident Jonas Dimoso, Makamu Mkuu wa Chuo Taaluma, Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini (IRDP), Dodoma;
- (iii) Bw. Said Abdallah Panga, Mkuu wa Idara ya Usimamizi wa Rasilimaliwatu, Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini (IRDP), Dodoma;
- (iv) Bw. Joseph Felix Chilambo, Meneja Uendeshaji Biashara, Benki ya Maendeleo ya TIB, Dar es Salaam; na
- (v) Bw. John Mihayo Cheyo, Mkurugenzi wa Sera na Mipango, Ofisi ya Rais.

Uteuzi huu umeanza tarehe 20 Oktoba, 2022.

(B): UTEUZI WA WATENDAJI:

- (i) Amemteua Prof. Tumaini Joseph Nagu kuwa Mganga Mkuu wa Serikali. Kabla ya uteuzi huu Prof. Nagu alikuwa Kaimu Mkuu wa Idara ya Tiba, Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS). Prof. Nagu anachukua nafasi ya Dkt. Aifello Sichelwe ambaye atapangiwa kazi nyingine.

Uteuzi wa Prof. Nagu umeanza tarehe 19 Oktoba, 2022.

- (ii) Amemteua Bw. Deusdedit Kamalamo Bwoyo kuwa Mkurugenzi wa Idara ya Misitu na Nyuki, Wizara ya Maliasili na Utalii. Bw. Bwoyo alikuwa Kaimu Mkurugenzi, Idara ya Misitu na Nyuki.

Uteuzi wa Bw. Bwoyo umeanza tarehe 20 Oktoba, 2022.

- (iii) Amemteua Bw. James Mahanga Sando kuwa Katibu Mtendaji wa Mamlaka ya Rufaa za Zabuni za Umma (*Public Procurement Appeals Authority - PPAA*). Bw. Sando alikuwa Mkuu wa Kitengo cha Fedha Kampuni ya *Crown Accounting and Consulting Firm*, Dar es Salaam.

Uteuzi wa Bw. Sando umeanza tarehe 20 Oktoba, 2022

Zuhura Yunus

Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu

